# Serikali yatoa miezi 3 uendeshaji nyama, maziwa

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (pichani), ametoa miezi mitatu kwa Msajili wa Bodi ya Maziwa nchini na Bodi ya Nyama, kuweka mikakati imara ya uendeshaji wa biashara katika bodi hizo.

Alitoa agizo hilo jijini Dar es Salaam alipokutana na Bodi ya Maziwa na Nyama kwa ajili ya kutoa maelekezo mbalimbali.

Ulega alisema mpaka sasa serikali inatumia pesa nyingi kila mwaka kuagiza maziwa nje ya nchi na kwamba endapo kungekuwa kumewekwa mazingira mazuri ya uzalishaji wa maziwa hayo nchini, badala ya fedha hiyo kutumika kuagiza bidhaa hiyo nje ingetumika kuboresha uzalishaji wa maziwa ya ndani.

"Maziwa mengi yanapotea huko kwa wafugaji, lakini moja ya sababu kubwa ya maziwa hayo kupotea ni kutokana na kutokuwapo kwa mipango mizuri ya namna ya kuyakusanya au kuyapata, kwa sababu vibebeo vyenyewe vya maziwa hayo ni gharama kubwa kwa hiyo wengi wao wanashindwa kumudu kuvinunua," alisema Ulega.

"Sasa nakuagizeni, changamkeni. Tunataka vibebeo vya maziwa viende huko kwa wazalishaji na mshirikiane na watu wa sekta binafsi, wenye viwanda vidogo na vikubwa kusambaza hizo, sambazeni vifaa vya kubebea maziwa kwa vikundi vya kinamama na vijana na mpite kwenye hizi halmashauri zenye mifugo," alisema Ulega.

"Tunataka hivi vikundi vya wafugaji vya kinamama na vijana watumie pesa zile za halmashauri za asilimia 10 wanazopewa wakusanye maziwa yaliyopo kule vijijini ili yachakatwe, kwa hiyo kitengo cha masoko mnatakiwa kuamka na kuleta matokeo makubwa."



Alisema serikali inatumia Sh. bilioni 14 kila mwaka kuagiza maziwa nje, na endapo kutakuwa na mipango mizuri, badala ya kiasi hicho cha fedha kutumika kuagiza bidha hiyo nje ya nchi, itatumika kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ndani ya upatikanaji wa maziwa kwa wingi.

Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. George Msalya, alisema uzalishaji wa maziwa nchini umeongezeka kutoka lita bilioni 3.1 mwaka 2019/2020 hadi lita bilioni 3.4 mwaka 2020/2021.

Pia alisema usindikaji wa maziwa hayo umeongezeka kutoka lita 203,600 kwa siku mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita 208,000 kila siku mwaka 2020/2021.

MWANANCHI

MWANANCHI.CO.TZ JUMATATU

UZALISHAJI



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) akizungumza wakati wa kikao chake na watendaji wa bodi ya maziwa na nyama kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Msajili wa bodi ya maziwa, Dk George Msalya na Kaimu msajili wa bodi ya nyama, John Chassam. Na Mpiga Picha Wetu

# Maagizo ya Ulega kwa bodi ya maziwa

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wakati Serikali ikipendekeza kufuta ongezeko la kodi ya thamani ya mikebe ya kuhifadhiwa maziwa, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameitaka bodi ya maziwa Tanzania kuweka utaratibu bora wa kutambua wafugaji wa ng'ombe wa maziwa watakaochangamkia fursa hiyo.

Mbali na hilo, Ulega aliagiza bodi ya nyama kuwatambua wafugaji, ili kuwawekea mikakati na njia bora itakayosaidia mifugo yao kunenepeshwa na kutoa nyama bora zitakazouzwa nje ya nchi.

Juni 10, mwaka huu wakati akiwasilisha bajeti kuu, Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba alipendekeza kutoa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kwenye mikebe ya kubebea maziwa, ili kupunguzia gharama wazalishaji na kuchochea ukuaji wa sekta ya maziwa. Katika bajeti hiyo, Mwigulu alipendekeza kutoza ada ya Sh 40,000 kwenye kibali cha kupeleka nyama nje ya nchi kwa nyama zote bila kujali aina ya nyama, badala ya ada ya Sh100 kwa kilo moja ya nyama ya ng'ombe na Sh 50 kwa kilo moja ya nyama ya mbuzi na kondoo.

Ulega alitoa maelekezo hayo juzi alipozungumza na wafanyakazi na viongozi wa bodi za nyama na maziwa zilizopo chini ya wizara hiyo. Alisema endapo bodi hizo zikifanikiwa kuweka mikakati bora ya kuwatambua wafugaji itasaidia kuwajengea mazingira ya kufanya biashara kwa ufanisi.

Alizitaka bodi hizo kufanya kazi kwa kushirikiana na Tamisemi kwa ajili ya kuwatambua wafugaji hao kina wanawake kwa ajili ya kuhamasisha kupewa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kupitia mapato ya ndani.

"Kumekuwa na upotevu mkubwa maziwa kwa sababu wafugaji hawana mikebe mahsusi ya kuhifadhia, ili kuipeleka katika kiwanda husika. Hii ni changamoto kubwa. Sasa Serikali inakwenda kuleta unafuu kwa kupunguza gharama ya mikebe hii.

Awali, Msajili wa bodi ya maziwa, Dk George Msalya alisema kwa mujibu takwimu zilizopo ni asilimia 3 ya maziwa yanayozalishwa na kufika kwenye viwanda kwa ajili ya kuchakatwa.

Alisema hatua hiyo inatokana kukosekana kwa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa bidhaa hiyo na gharama kubwa ya mikebe ya kuhifadhia.

Scanned with CamScanner



# NARCO yaonyeshwa fursa uzalishaji malisho ya mifugo

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeshauri Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuanza kuzalisha malisho ya mifugo ili kusaidia wafugaji wanaozunguka ranchi hizo.

Akizungumza jana kwenye semina iliyoandaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kampuni hiyo kwa ajili ya kuwajengea uelewa wajumbe kuhusu majukumu ya NARCO, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alisema sasa ni wakati muafaka kwa Ranchi za Taifa kuanza kuzalisha malisho.

Aidha, alishauri ranchi hizo zitumike kama mashamba darasa ambapo wafugaji hasa wa maeneo ya jirani watapata elimu juu ya ufugaji bora.

Akichangia katika semina hiyo, Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema kamati hiyo inapaswa kuisaidia NARCO.

Alisema tayari kampuni hiyo imeshaandaa andiko mradi, ni vema wajumbe hao wakalisoma hilo andiko na kuona ni maeneo yapi kamati inaweza kuisaidia ili NARCO ipate mafanikio.

"Niwasihi NARCO kuendelea kuyatunza na kuyalinda maeneo yao kwani yanawasaidia wafugaji wenye changamoto ya maeneo ya malisho kwa kuwakodishia," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema wizara imeamua kufanya semina kuhusu NARCO ili wajumbe wa kamati hiyo wapate uelewa na kutoa maoni yao ambayo yatasaidia kuimarisha kampuni hiyo kwa kuongeza uzalishaji wa mitamba, nyama na kuzidi kuchangia kwenye pato la taifa.

Alisema kampuni hiyo ilipita katika kipindi kigumu na hivyo kushindwa kujiendesha lakini kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na wizara kwa sasa kampuni hiyo inajiendesha yenyewe.

Awali taarifa iliyowasilishwa kwa kamati, ilainisha mafanikio yaliyopatikana, mipango iliyopo ya kuongeza uzalishaji na maeneo ya vipaumbele yaliyopo katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ikiwamo kuboresha ranchi tano za Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi na West Kilimanjaro ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo.

Pia ilieleza mikakati ya kudhibiti vifo vya mifugo kwa kiwango kisichozidi asilimia mbili ya wastani wa mifugo, kuongeza na kuboresha nyanda za malisho kwa kudhibiti na kuondoa vichaka na kuimarisha vyanzo vya maji na kuweka alama za kuonekana katika mipaka ya ranchi, kuondoa wavamizi na kuimarisha ulinzi wa mipaka.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.10, Tarehe 14/06/2021

# Serikali yafungua mnada uliofungwa miaka 20

**Na Mbaraka Kambona**, MARA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameielekeza Halmashauri ya Mji wa Tarime kuifungua mnada wa mpakani wa Magena uliofungwa kwa zaidi ya miaka 20 ili uanze kufanyakazi ya biashara ya mifugo kama ilivyokusudiwa hapo awali.

Waziri Ndaki alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya siku moja aliyoifanya mkoani Mara mwishoni mwa wiki, alipotembelea kuona hali ya mnada huo na kuruhusu uanze kufanya kazi baada ya kuelezwa na kujiridhisha kuwa sababu zilizosababisha mnada huo kufungwa hazipo tena.

"Leo nimekuja kuufungua mnada huu wa Magena uanze kufanya kazi mara moja, ninaelekeza kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime na watendaji katika ngazi ya wizara yangu wakutane haraka ili wapange siku ambayo mnada huu utaanza kufanyakazi, na hiyo taarifa nipewe ndani ya wiki moja," alisema Ndaki.

Alisema serikali imedhamiria kuufanya mnada huo kuwa wa kimataifa na watahakikisha wanaboresha miundombinu yote iliyochakaa ili iweze kutoa huduma nzuri na serikali ianze kukusanya mapato yake.

"Kwa kuanzia tumetenga Sh. milioni 150 kwa ajili ya kuanza kuboresha miundombinu ya mnada huu na tutaendelea kuuboresha zaidi ili uweze kuvutia watu wengi wakiwemo kutoka nchi za jirani kuja kufanya biashara hapa," alisema Ndaki.

Aidha, aliwataka wananchi wa Wilaya ya Tarime, hususan wanaoishi katika Kijiji cha Magena, kuhakikisha wanautunza mnada huo ili uweze kuwa na tija kwao pamoja na nchi kwa ujumla.

Aliwaonya wenye tabia ya wizi wa mifugo kuacha vitendo hivyo kwa kuwa ndiyo vilichangia mnada huo kufungwa, na kwamba serikali ipo imara na imejipanga kuhakikisha wanakomesha vitendo hivyo ili wafanyabiashara wa mifugo waweze kuutumia mnada huo na kufanya shughuli zao kwa amani.

"Serikali imedhamiria kuboresha maisha ya wananchi wake, kufunguliwa kwa mnada huu ni katika jitihada za kuboresha maisha yenu ili kila mmoja aweze kupata maendeleo yake kupitia shughuli halali anazozifanya," alifafanua Ndaki.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ambaye ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alisema kufunguliwa kwa mnada huo kutatoa fursa kwa wananchi wa mkoa huo kujiongezea kipato kupitia shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinaendelea katika mnada huo.

"Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa kutufungulia mnada huu, lakini nakuomba usiishie kuwa mnada wa mpakani tu, ni muhimu tukauboresha kwa kujenga miundombinu ya kisasa ili uwe wa kimataifa na serikali iweze kukusanya mapato mazuri na wananchi pia waweze kufaidika kupitia rasilimali zao," alisema Waitara.

Alisema ni muhimu operesheni inayoendeshwa na Jeshi la Polisi nchini ya kupambana na wizi itumike pia kushughulika na wezi wa mifugo ili biashara hiyo iweze kwenda vizuri na kushamiri mkoani humo.

Mnada huo ulikuwa kati ya minada 10 ya mipakani na ulijengwa mwaka 1995 na kufunguliwa mwaka 1996 na kufanya kazi kwa mwaka mmoja kabla ya kufungwa kwa sababu zilizotajwa ikiwamo wizi wa mifugo na sababu nyingine za kiusalama na kusababisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo kuufunga Mei 14, 1997.

Scanned with CamScanner

# TGNP: Serikali imedhamiri kuweka usawa wa kijinsia

Na David John

■■ MKURUGENZI wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi amesema Serikali ya Rais, Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuweka usawa wa kijinsia kwa kuangalia nyanja tano za maendeleo ikiwemo maji, usafiri, elimu, afya na uzinduaji kupitia bajeti ya fedha ya mwaka 2021/22.

Aliitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika kikao

# Serikali yaufungua Mnada wa Magena

Na Mbaraka Kambona, Mara

■■ WAZIRI Nwa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ameielekeza Halmashauri ya Mji wa Tarime kuufungua mnada wa mpakani wa Magena, uliofungwa kwa zaidi ya miaka 20 ili uanze kufanya kazi ya biashara ya mifugo kama ilivyokusudiwa awali.

Waziri Ndaki alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya siku moja aliyoifanya mkoani Mara mwishoni mwa wiki, ambapo alitembelea kuona hali ya mnada huo na kuruhusu uanze kufanya kazi, baada ya kuelezwa na kujiridhisha kuwa zile sababu zilizosababisha mnada huo kufungwa hazipo tena.

"Leo (Jumamosi) nimekuja kuufungua mnada huu wa Magena, uanze kufanya kazi mara moja, ninaelekeza kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime na watendaji katika ngazi ya wizara yangu, wakutane haraka ili wapange siku ambayo mnada huu utaanza kufanya kazi na hiyo taarifa nipewe ndani ya wiki moja," alisema.

Alisema kuwa serikali imedhamiria kuufanya mnada huo kuwa wa kimataifa na watahakikisha, wanaboresha miundombinu yote iliyochakaa ili iweze kutoa huduma nzuri na serikali ianze kukusanya mapato yake.

"Kwa kuanzia tumetenga sh. milioni 150 kwa ajili ya kuanza kuboresha miundombinu ya mnada huu na tutaendelea kuuboresha zaidi, ili uweze kuvutia watu wengi wakiwemo kutoka nchi za jirani kuja kufanya biashara hapa," alisema.

Aliwataka wananchi wa Wilaya ya Tarime, hususan wanaoishi katika Kijiji cha Magena kuhakikisha wanautunza mnada huo ili uweze kuwa na tija kwao pamoja na nchi kwa ujumla.

Waziri Ndaki aliwaonya wenye tabia ya wizi wa mifugo, kuacha vitendo hivyo mara moja kwani ndiyo vilichangia hata mnada huo kufungwa, huku akisema serikali ipo imara na imejipanga kuhakikisha wanakomesha vitendo hivyo ili wafanyabiashara wa mifugo, waweze kuutumia mnada huo na kufanya shughuli zao kwa amani.

"Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kuboresha maisha ya wananchi wake, kufunguliwa kwa mnada huu ni katika jitihada za kuboresha maisha yenu ili kila mmoja aweze kupata maendeleo yake kupitia shughuli halali anazozifanya," alifafanua.

Naye Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ambayo pia ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara alisema kufunguliwa kwa mnada huo kutatoa fursa kwa wananchi wa Mkoa wa Mara kujiongezea kipato kupitia shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinaendelea katika mnada huo.

"Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa kutufungulia mnada huu, lakini nakuomba usiishie kuwa mnada wa mpakani tu ni muhimu tukauboresha kwa kujenga miundombinu ya kisasa kwa ajili uwo wa kimataifa ili serikali, iweze kukusanya mapato mazuri na wananchi pia waweze kufaidika kupitia rasilimali zao," alisema Waitara.

Aliongeza kuwa ni muhimu sasa operesheni inayoendeshwa na Jeshi la Polisi nchini la kupambana na wizi, itumike pia kushughulika na wezi wa mifugo ili biashara hiyo iweze kwenda vizuri na kushamiri mkoani hapa.

Mnada huo wa Magena ulikuwa kati ya minada 10 ya mipakani na ulijengwa mwaka 1995 na kufunguliwa mwaka 1996, ambapo ulifanya kazi takribani mwaka mmoja kabla ya kufungwa kwa sababu zilizotajwa kukithiri wakati huo, ikiwemo wizi wa mifugo na sababu nyingine za kiusalama zilizosababisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kuufunga Mei 14, 1997.

Scanned with CamScanner

Majira Uk. 16, Tarehe
14/06/2021



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Magena (hawapo pichani) alipotembelea Mnada wa Magena uliopo wilayani Tarime Mkoa wa Mara jana.** (Picha na Ikulu)

Scanned with CamScanner

# Bodi ya Maziwa yapewa mbinu

**Vicky Kimaro**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameitaka Bodi ya Maziwa Tanzania (BMT) kuweka mikakati ya upatikanaji wa keni za kubebea maziwa ili kusaidia ukusanyaji wa bidhaa hiyo kwa urahisi nchini.

Alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam jana alipokutana na viongozi na wakuu wa idara kutoka BMT na Bodi ya Nyama Tanzania.

Alisema hivi karibuni katika Bajeti Kuu ya Serikali yapo mapendekezo ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye keni za maziwa kwa lengo la kuweka unafuu kwenye bidhaa hiyo.

Alisema lengo ni kurasimisha tasnia ya maziwa na kuongeza fursa za biashara kwa wazalishaji nchini.

Aidha, aliitaka Bodi ya Maziwa kushirikiana na viwanda vya maziwa, Tamisemi na wabia wa maendeleo katika kuhakikisha hamasa kubwa inatolewa ili kuongeza uzalishaji na usambazaji wa keni kwa wingi nchini baada ya kuwapo kwa unafuu unaopendekezwa.

"Bodi ya Maziwa tunataka mshirikiane na viwanda vikubwa, vya kati na vidogo katika kuhakikisha keni za maziwa zinaenda kwa wingi kwa wadau na hasa akinamama na vijana katika halmashauri zetu nchini," alisema.

Uliga aliitaka BMT iwashawishi wakurugenzi wa halmashauri na kwa kushirikiana na wataalamu wa Tamisemi wakiwemo maofisa mifugo, maofisa ushirika na maofisa maendeleo ya jamii kuhakikisha asilimia 10 ya mapato ya mifugo inatolewa kwa akinamama na vijana kama mikopo kwa ajili ya tasnia ya maziwa na fedha hizo zisaidie kununua keni na ukusanyaji wa maziwa.

Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Dk George Msalya alisema kwa takwimu zilizopo, takribani asilimia tatu ya maziwa yanayozalishwa nchini yanafika viwandani kwa ajili ya kuchakatwa na hivyo yanayoingia katika mfumo ulio rasmi ni kidogo.

Dk Msalya alisema hali hiyo inatokana na kukosekana kwa mifumo mizuri ya ukusanyaji wa maziwa na gharama kubwa ya ununuzi wa vifaa vya kukusanyia zikiwamo keni.

Alisema kwa nafuu inayotolewa, bodi inajipanga keni zipatikane kwa wingi na kuwafikia akinamama na vijana kama alivyoagiza Naibu Waziri huyo.

Scanned with CamScanner

# Waitara asimamisha vivuko vya kampuni ya Kamanga

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, amesimamisha huduma za vivuko viwili vinavyomilikiwa na kampuni ya Kamanga Ferry Limited hadi vitakaporekebisha kasoro zilizobainika.

Alikuwa ameongozana na wadau wengine wa usafirishaji mkoani hapa mwishoni mwa wiki, wakiwemo wa Kampuni ya Huduma za Meli

# Nyavu, zana za uvuvi haramu zateketezwa

**Na Yohana Shida, Geita**

MKUU wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho ameteketeza nyavu na zana nyingine za uvuvi haramu zenye thamani ya Sh milioni 66.1 ikiwa ni mwendelezo wa vita dhidi ya uvuvi haramu ndani ya Ziwa Victoria.

Kabeho katika mazungumzo na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, alisema uvuvi haramu umekuwa kikwazo kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi nchini.

Alisema baadhi ya nyavu zilizoteketezwa ziliIetwa na wananchi waliotii agizo la kuwasilisha kwa hiyari zana haramu za uvuvi na ningine zikapatikana kutokana na msako unaoendelea.

Kwa mujibu wa Kabeho, msako ni endelevu na hautakomea kwa wavuvi wenye zana hizo pekee, bali kamati ya ulizi na usalama ya wilaya itafanya doria majini na sokoni kubaini wanaouza samaki wachanga ili wachukuliwe hatua za kisheria.

"Pia kuna wengine wanasafirisha samaki wadogo kwa bodaboda, nimeshazungumza na Mkuu wa Polisi Wilaya. Tutaanza kuwakamata hadi wale wanaosafirisha, lakini tukiona bado watu hawatuelewi, tutaanza kukamata na yule anayekwenda kununua samaki wachanga kwani nao wanachochea uvuvi haramu," alisema.

Awali akitoa taarifa ya msako huo, Ofisa Mifugo na Uvuvi Wilaya, Dk Elphas Msenya, alisema miongoni mwa zana haramu zilizokamatwa ni pamoja na makokoro 29 yenye thamani ya Sh milioni 26 .1, matimba 366 ya Sh milioni 32.9, makira 40 ya Sh milioni 1.6 pamoja na kamba



za makokoro mita 250 za Sh 375,000.

Msenya alizitaja zana zilizokamatwa kwamba ni tupatupa tatu zenye thamani ya Sh 150,000, dududu nne za Sh milioni 4.8, katuli 12 za Sh 84,000 na migono miwili ya Sh 60,000.

Mwenyekiti wa Kata ya Chato, ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa Umoja wa Kusimamia Fukwe za Ziwa Victoria (BMU), Batazar Malima, aliwahimiza wananchi kuendelea kuwasilisha zana haramu kabla ya kufikwa na msako ili kuunga mkono juhudi za kuendeleza uvuvi salama na kuepuka mkono wa sheria.

Scanned with CamScanner

14/06/2021



The Guardian



# Govt advises NARCO to start livestock fodder production

By Guardian Correspondent, Dodoma

AGRICULTURE, Livestock and Water Parliamentary Committee has advised the National Ranching Company (NARCO) to start producing livestock fodder to assist herders near its ranches.

Speaking here yesterday at a seminar organised by the Livestock and Fisheries Ministry through NARCO aimed to empower delegates in attendance to understand the company's responsibilities, the Committee's Chairman, Dr Christine Ishengoma said it was the right time for the state owned ranches to start producing animal fodder.

She advised the ranches to be used as demonstration farms for herders in the ranches' vicinities to be provided with better livestock keeping practices. Contributing to the seminar debate, Moshi Rural Member of Parliament, Prof Patrick Ndakiemi said the panel was supposed to assist NARCO.

He said already NARCO has already prepared a project document, hence it would be better they read it and see which areas could assist to enable the company attain its achievements.

"I beseech on you to continue taking care of your ranch areas as they assist herders facing challenges on grazing areas by renting them," he said.


For his part, Deputy Livestoc\k and fisheries Minister Abdallah Ulega said the Ministry has decided to hold the seminar on NARCO to enable panel members understand on the issue and give their views that would help to strengthen the company and be able to increase the production of meat and quality livestock breeds to contribute to the national income.

Earlier, a report submitted to the panel spelled out NARCO's achievements, current production plans and priority areas in the 2021/22 Budget, including revamping of five ranches - Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi and West Kilimanjaro in order benefits in the entire value chain for livestock products.

The report also spelled out strategies for the control of livestock deaths at not more than two per cent, to increase and improve grazing areas, to erect visible ranches' boundaries, improve water sources and evict invaders from ranch areas.

Scanned with CamScanner

Habari Leo Uk.5, Tarehe 14/06/2021



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Gabriel akifafanua jambo wakati wa Semina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu majukumu, muundo, mafanikio, changamoto na mikakati ya kutatua changamoto zinazoikabili Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) iliyofanyika katika viwanja vya Bunge Dodoma mwishoni mwa wiki. (Picha na Iddy Mwema).

Scanned with CamScanner